# MUNGU

# ANANIPENDA

KIMEANDIKWA NA
KEITH MOORE

# Mungu Ananipenda

**KIMEANDIKWA NA KEITH MOORE**

MUNGU ANANIPENDA

Hakimiliki 2018 Keith Moore
Ilichapishwa tena 2022, 2020

ISBN: 978-1-940403-01-4

BKS25

Moore Life Ministries
6009 Business Boulevard
Sarasota, Florida 34240
941-702-7390
www.mlm.org

Iwapo hayajaonyeshwa vingine, manukuu yote ya Maandiko katika kitabu hiki yanatoka katika biblia ya Common English Version iliyo katika lugha ya Kiingereza.

# Mungu Ananipenda

Wagalatia 5:6 inasema, “Kutahiriwa au kutokutahiriwa si jambo la maana katika Kristo Yesu, bali imani itendayo kazi kwa upendo inahusika.” Si mambo ya nje—sherehe za kawaida au matendo ambayo yana thamani. Ni imani ambayo ina thamani. Mstari huo unasema, “Imani itendayo kazi kutokana na upendo,” au kama vile Amplified Bible inavyosema, “Imani inayochochewa…kupitia upendo.” Tafsiri nyingine inasema, “Imani itendayo kazi kwa upendo.” Imani hufanya kazi kwa upendo. Inafanya kazi na inachochewa na upendo. Je, kuna uhusiano kati ya imani na upendo? Ikiwa upendo haufanyi kazi, je, hilo litaathiri imani? Ndiyo, bila shaka. Kwa hiyo tunapaswa kufikiria juu ya upendo tunapofikiria juu ya imani, kwa sababu imani hufanya kazi kupitia upendo.

Kama upendo haupo kama inavyopaswa kuwa, basi imani haitafanya kazi jinsi inavyopaswa kufanya kazi.

1 Yohana sura ya 4 ni kifungu cha ajabu juu ya upendo. Mstari wa 7 hadi 9 unasema, “Wapenzi, na tupendane, kwa maana pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu. Mtu asiye na upendo hamjui Mungu, kwa maana Mungu ni upendo. Hivi ndivyo upendo wa Mungu unavyodhihirishwa kwetu: Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni ili tupate uzima kupitia yeye. Kulikuwa na—na kuna—udhihirisho wa upendo wa Mungu. Mstari wa 10 unaendelea, “Huu ndio upendo: si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi hadi akamtuma mwanawe kuwa dhabihu itakayotukomboa kutoka kwa dhambi zetu. Wapenzi, ikiwa Mungu alitupenda hivi, pia sisi tunapaswa kupendana.”

1 Yohana 4:17 inasema, “Hivi ndivyo upendo umekamilishwa ndani yetu, ili tuwe na ujasiri Siku ya Hukumu, kwa maana sisi ni sawa kabisa na Mungu katika ulimwengu huu. Je, kuna uhusiano kati ya upendo na ujasiri? Je, kujiamini na ujasiri vinahusishwa na imani? Ndiyo, na vyote vinaunganishwa na upendo. Anafafanua zaidi katika mstari wa 18. "Hakuna hofu katika upendo ..." Hakuna hofu. Ikiwa hungekuwa na woga kabisa bali mwenye imani na ujasiri tu, je, ungekuwa katika imani? Ndiyo, na hayo ni matokeo ya upendo. Anaendelea kusema, “Upendo mkamilifu,” au kamili, “hutupilia mbali hofu.” Neno *tupilia mbali* lina uzito mkubwa. Linamaanisha “kutupa kitu bila kujali kitatua wapi,” na ndivyo upendo unavyofanya kuelekea uoga. Upendo hutupilia mbali hofu. Hilo, linanipendeza. "Upendo mkamilifu hufukuza woga, kwa sababu hofu hutarajia kuwapo kwa mateso." Hofu hutesa. Unapoogopa gharama za nyumbani kwako hazitalipwa, hofu inaathiri akili yako unapojaribu kufanya kazi, au unapojaribu kufanya mambo nyumbani. Na hofu huathiri mahusiano yako.

Watu wengi wako chini ya shinikizo na dhiki kwa sababu ya shinikizo la kifedha, na ni hofu tu kwamba hawatafanikiwa. Wanakuwa na hofu kwamba pesa hazitakuwepo kwa wakati, au kwamba hazitatosha. Au wanaweza kuwa na hofu kuhusu miili yao—kwamba haitaboreka au itazidi kuwa mibaya zaidi. Wanahofia kwamba watakufa katika umri wa makamo, au kwamba watakufa kabla ya wakati.

Ukiiruhusu, hofu hiyo itakuwa nawe wakati wote wa kuamka. Itakuamsha katikati ya usiku. Hili linatesa, na halitokani na Mungu. Mungu hakutupa roho ya woga.

**Mungu Ananipenda**

Nini kitaondoa hofu? Upendo kamili. Upendo kamili utautupilia mbali hofu. Upendo utatupilia mbali hofu na kuuondoa ili uwe na ujasiri tu. Hilo linanipendeza, je wewe? Upendo wa Mungu na imani ya Mungu haviwezi kutenganishwa. Havitenganishwi katika utendaji.
Paulo alisema katika 2 Timotheo 1:12, "…Namjua yeye niliyemwekea imani yangu. Nimesadikishwa kwamba Mungu ana nguvu za kutosha kulinda kile ambacho ameweka katika tumaini langu hadi siku hiyo." Namjua ambaye nimemwamini. Imani sio tu kushikamana kiakili na kanuni au desturi za kisheria au utaratibu. Imani inahusisha kumjua aliyetamka maneno hayo. Ninamjua. Sijui yote kumhusu, lakini ninamjua, na yeye ananijua. Ninajua mambo ya kutosha kumhusu, na ninaamini kwamba kama alivyosema, tunaweza kutegemea, na tunaweza kuweka msingi juu ya hayo. Tunaweza kuyategemea. Kumjua ni kuujua upendo, kwa sababu Mungu ni upendo.

Mara nyingi watu wanaposikia usemi "upendo mkamilifu huutupilia mbali hofu" au "imani hufanya kazi kupitia upendo," wanafikiri kwamba unarejelea kutenda kwa upendo—kwamba ikiwa watatenda kwa upendo, imani yao itafanya kazi. Hilo hakika ni ukweli, na hiyo ni sehemu yake, lakini yeye hakusema hivyo *tu* , na hakuweka *kikomo* kwa hilo. Alisema kwamba imani hufanya kazi kupitia upendo katika ukamilifu wake. Kwa hivyo usiihusishe mistari hii tu na kutembea kwa upendo na wengine na jinsi hilo linavyoathiri imani yako. Ni hakika, lakini kwanza kabisa, unahitaji kuelewa ni kwa kiasi gani Mungu anakupenda.

Upendo wa Mungu kwako, upendo wako kwa Mungu, upendo wako kujielekea, na upendo wako kwa wanadamu wenzako vyote vinafanya kazi pamoja katika utendaji wa imani. Kitu ambacho kinaendelea kuweka imani yangu hai ni ufunuo mkuu kuhusu jinsi anavyonipenda. Ninapoanza kuona jinsi anavyonijali sana, imani yangu hujitokeza, na ninajua nitafanya hivyo—si kwa sababu mimi si wa kawaida, bali kwa sababu ananipenda. Nina mtu mkubwa upande wangu.

Miaka mingi iliyopita, nilikuwa na mbwa wa aina ya Doberman, uzao halisi wa Doberman. Nadhani alikuwa na uzito wa karibu ratili 110. Ni mbwa ambaye hungependa kukutana naye usiku. Alikuwa mbwa mkubwa, mwenye kutisha, na alikuwa mbwa *wangu* , kwa hiyo nilikuwa sawa. Lakini wageni hawakuwa sawa. Mbwa huyu alikuwa nami wakati wote. Aliandamana nami kwenye gari langu, alikuwa akiukamata mpira wa Frisbee ® nilipokuwa nacheza naye , na alilinda vitu vyangu. Lakini ikiwa wageni wowote walikuja kwangu, ilibidi niwe makini, la sivyo angewavamia—na hata asingewaonya. Angewanyemelea tu nyuma yao, na lifuatalo ni kwamba, angewauma.

Siku moja wauzaji fulani walikuja kwangu. Sikujua, lakini walikuwa wamekuja kwa gari. Mbwa wangu alilizunguka gari na kunyemelea nyuma yao. Walikuwa wameyafungua madirisha wazi, kisha akaingiza kichwa chake ndani, akawatazama, na kunguruma. Nilidhani wangehepa kupitia paa la jua kwenye gari lile! Waliondoka na hawakurudi.

Wakati mwingine, rafiki alikuja na kumleta mtoto wake mdogo. Nadhani mvulana huyo alikuwa na umri wa miaka miwili au mitatu hivi. Walishuka kwenye gari, na mbwa wangu alikuwa hapo. Kwa kweli, mtoto huyu mdogo aliogopa. Ni wazi! Mbwa huyo alionekana mwenye kuogopesha sana—na *alikuwa* wa kuogofya. Lakini baba yake alikuwa mtu mkubwa, na mvulana mdogo akakimbia nyuma ya baba yake na kuchungulia kutoka nyuma ya mguu mmoja wa babake.

Nilimwongelesha mbwa wangu, kisha nikawaambia watakuwa sawa. Rafiki yangu alifika karibu na kumchukua mvulana wake mdogo na kusema, "Usijali kuhusu hilo, mwanangu. Sitamruhusu akusumbue. Yuko mtulivu. Twende." Kwa hiyo mvulana mdogo alitoka nyuma na kuenda mbele yake. Sasa, alikaa karibu ambapo angeweza kumgusa baba yake, lakini mara moja, alipata ujasiri fulani. Nilitazama woga wake ukipotea, naye akasogea, alimkaribia na, na kumgusa yule mbwa kwenye pua—lakini aliuweka mkono mmoja nyuma ambapo angeweza kumgusa baba. Kwa nini hofu yake ilitoweka? Kwa sababu babake mkubwa alikuwa amezungumza naye na kusema, "Ni sawa, mwanangu."

Sasa hili ndilo ninalotaka uelewe: Baba yake hakumwambia, "Sasa mwanangu, ninakupa ahadi: sitamwacha mbwa huyu mkubwa, mbaya akuvamie." Hakusema maneno hayo. Alisema tu, "Njoo nami," na mvulana huyu mdogo alijua ya kwamba baba yake alimpenda, kwa hiyo haikumbidi kusema maneno hayo. Alijua kwamba angekuwa mwangalifu, angemlinda, na angemtunza kwa sababu alijua kwamba anampenda.

*Unapojua* kwamba Mungu anakupenda, itakuondolea maswali mengi. Itakuondolea mfadhaiko na hali ya kukosa msimamo. Watu wanapouliza, "Je, Mungu ataniponya?" hawajui ni kiasi gani anawapenda, au hawangeuliza swali. "Je, Mungu atanisaidia kulipa gharama zangu za nyumbani? Je, Mungu atawacha nilemewe? Niko nyuma. Je, Mungu atanisaidia nifutilie mbali deni langu? Sijui—unafikiri ni mapenzi yake?" Kuuliza hivyo kunamaanisha kuwa humjui. Sijasema hujaokoka, lakini humjui kabisa, maana kama ungejua jinsi anavyokupenda, usingeuliza hivyo.

Haitoshi tu kuwa na imani katika uwezo wake. Je, unamkumbuka mwenye ukoma kwenye Marko 1:40? Alimwambia Bwana, "Ukipenda, najua unaweza kunitakasa." Alikuwa na hakika kwamba Bwana *angeweza* kufanya hivyo, lakini hakujua kama *angefanya* hilo. Hivyo ndivyo wakristo wengi wanaamini. Wanaamini kwamba Mungu ana uwezo wa kuponya, au uwezo wa kukidhi mahitaji yao, lakini hawajashawishika kwamba atafanya hivyo kwa ajili yao. Hakuna tofauti yoyote ni uwezo kiasi gani au rasilimali kiasi gani mtu anamiliki; kama huna uhakika kwamba hivi vitatumiwa kwa ajili yako, huwezi kuwa na imani ya kupokea.

Lakini unapojua jinsi Mungu anavyokupenda, unajua kwa nini anatumia uwezo wake na kwa nini alituumba. "Yeye hupendezwa na upendo mshikamanifu," kama vile andiko la Mika 7:18 linasema. Anataka kufanya hayo. Anafurahia kuyatenda. Hio ni *kawaida* yake. Unaweza kuuliza, "Unamaanisha nini kwa kusema hivyo?" Naam, Mungu anapenda kufanya nini? Una mambo fulani ambayo unapenda kufanya, lakini Mungu anapenda kufanya nini? Anafurahia kuonyesha rehema—hicho ndicho anachofurahia. Inamfanya Mungu aseme, *Naam! Ninafurahia hili!* Mtu anapomwamini, au mtu anapofungua mlango na kumwacha awafanyie kile anachoweza kufanya. Macho yake yanatazama duniani nzima, pande moja mpaka nyingine—na Mungu ana darubini nzuri. Anaichambua dunia, akitafuta mtu aliye na moyo kamili kumwelekea. Anatafuta mtu anayeamini, ili aweze kujionyesha kuwa mwenye nguvu kwa niaba yao na kuwafanyia baadhi ya mambo fulani "ya ukubwa wa Mungu". ( 2 Mambo ya Nyakati 16:9 ) Anapoweza kufanya hivyo, yeye husema, "Naam! Hilo limenipendeza." Anaifurahia.

Ibilisi amelidanganya Kanisa na ulimwengu mzima kuhusu Mungu. Mengi ya makanisa yamesisitiza kwamba Mungu hahusiki kabisa na wanadamu. Aliiumba na hakutilia maanani, na

ameenda mahali fulani fulani ili kuitazama tu, akijua tutaivuruga, huku akingoja tu hadi siku ya hukumu ifike. Wengi ulimwenguni wanahisi hivyo kumhusu Mungu kwa sababu ya kile ambacho Kanisa limesema.

Lakini Mungu anatupenda. Kwa kweli, anatupenda sana. Anatujali. Anafuatilia mambo kama idadi ya nywele kwenye vichwa vyetu. ( Mathayo 10:30 ) Sihesabu nywele kwenye kichwa changu. Je, wewe hufanya hivyo? Sihesabu nywele kwenye vichwa vya wapendwa wangu. Je, wewe hufanya hivyo? Lakini yeye anafanya hivyo.

Watu wengine ni wasahaulifu katika mawazo yao na wao husema, "Nashangaa ikiwa Mungu anajali kiasi hicho." Hata watu ambao wana msingi mzuri katika imani wanamhoji. Wakati mambo yanapoendelea kutokea na hayabadiliki au kutokea haraka, adui atawashawishi na kusema, “Mungu hajali kabisa. Kama kweli anajali, angelifanya jambo kuhusu hili. Kama kweli anajali, hili lisingeendelea kwa muda mrefu hivi. Hali haingekuwa ilivyo sasa.” Usiruhusu kamwe uwe na mawazo kama haya! Ni uongo!

Mungu anakujali, na ikiwa utachunguza kwa kina, utaona kwamba amekuwa na huruma zaidi kwako kuliko vile ungemwomba akufanyie. Mara nyingi huwezi kuona mambo kwa undani. Amesikia maombi yako. Anaheshimu imani yako. Anakufanyia mambo. Amefanya mambo kwa ajili yako. Ana mpango mzuri kwako. Na kama utakaa tu Naye, utaishia mahali pazuri.

Lakini shetani anajua hilo, hivyo anataka kuvuruga na kuzuia ushirika wako. Hata kama hauulizi mambo kwa sauti kubwa, anataka maswali haya yawe yanakusumbua katika akili yako: “Kwa nini Mungu amefanya hivyo? Kwa nini aliruhusu hili? Kwa nini aliruhusu hili litokee? Kwa nini hajafanya hili au lile? Sielewi.” Ni sawa kuwa na maswali, lakini *si* sawa kuwa na shaka na upendo Wake. Na *si* sawa kuwa na hoja na uaminifu wake.

Kumbuka wanafunzi walipokuwa ndani ya mashua, na Yesu alikuwa amelala nyuma kwenye mto. Dhoruba ikatokea. Ilikuwa kali mno. Hatimaye wanafunzi walimwendea Yesu, wakamtikisa na kusema, “Yesu! Yesu, inuka! Je, hujali kwamba tunakufa? Je, hujali kwamba tunaangamia?” Aliinuka na kushughulikia hali hiyo, lakini aliwatazama na kusema, “Mbona mnaogopa sana? Inakuwaje hamna imani?” ( Marko 4:37-40 ) Je, unaweza kujibu swali hilo? Kwa nini walijawa na hofu? Kwa nini hawakuwa katika imani? Walikuwa na shaka na upendo wake. Hawakufanywa wakamilifu katika upendo, na walikuwa wakihoji, “Mungu, je, hujali? Yesu! Utakuwa umelala huku wote tukizama? Je, hujali?” Hayo ni matusi kwa Mungu.

Daima kaa upande wa Mungu. Wakati hujui jambo, na wakati huelewi kwa nini, hata kwa machozi na maswali yako, mtazame Mungu na kusema, “Bwana, sielewi, lakini najua haya: Wewe ni mwaminifu kwangu. *Umenipenda* , na *Utanipenda* , na hutakosa kunitegemeza *kamwe* . Macho yangu yako kwako. Ninakutumaini wewe. Nakutegemea wewe.” Anakupenda.

Ninakuambia, kadiri unavyoelewa hili, ndivyo imani yako itakavyoanza kuwa dhabiti. Jambo la pili unalojua, jambo hilo ulilolikimbia litakuwa ni jambo unaloweza kulikaribia moja kwa moja, mbele ya baba yako, na kuligusa kwenye pua lake kama yule kijana na mbwa wangu. Utalitazama machoni. Utashughulika nalo. Utalishinda. Lakini daima weka kimfano mkono

mmoja juu ya Baba. Unajua yeye yuko pamoja nawe. Unajua anakuunga mkono. Mungu anakupenda.

Haitoshi kujua tu kwamba *anaweza* kufanya jambo fulani. Inakupasa kushawishika kwamba *atatumia* uwezo na rasilimali zake kwa ajili yako. Sio lazima ufanye muungamo wa dhambi kwa kupindukia, ukiwa na hoja na kuogopa ikiwa hutafanya hivyo mara kadhaa kwa siku, utahukumiwa kuzimu, hilo halitakusaidia. Hapana! Vipi kama hujatilia maanani kwa kina kila kitu? Bado anakupenda. Anaujua moyo wako. Ikiwa unatembea katika nuru uliyo nayo na kufanya vizuri zaidi unavyojua kufanya, hata kama hujui vya kutosha, atakuonyesha mengine zaidi. Ukifanya kosa, yeye atakurekebisha.
Nina hakika kwamba Keith Moore atafanikiwa, na unahitaji kusadikishwa kuwa *utafanikiwa*! Nina hakika kwamba nitakimbia shindano langu lote. Nitamaliza kozi yangu yote kwa furaha. Nitavuka mstari na kupiga utepe. Unajua kwa nini? Kwa sababu Mungu ananipenda.

Hayo yalikuwa madai ya mtume Yohana ili apate umaarufu. Je, unakumbuka Mungu alipomtumia kuandika Injili ya Yohana? Badala ya kujiita "Yohana" au "Yohana, mtume," alijiita "mwanafunzi ambaye Bwana alipenda." Tunamzungumzia nani? Yohana. Ni yupi mwanafunzi aliyeweka kichwa chake kifuani mwa Yesu? Alikuwa ni mwanafunzi ambaye Bwana alimpenda. Badala ya kusema "Yohana," alibadilisha jina lake.

Jina lako ni nani? Wewe pia unaweza kusema, "Mimi ni mfuasi ambaye Bwana anapenda."

Ingekufaidi zaidi ikiwa ungefanya kama Yohana. Wewe ni nani? Mimi ndiye anayempenda. Hatusemi kwamba hapendi mtu mwingine yeyote. Siwezi kuwa mtu wa kuamini kwamba anakupenda *kwa niaba* yako. Siwezi kuwa mtu wa kuamini kwamba anakupenda *kwa niaba* yako. Sema: **"Ananipenda."** Sema hivyo kila mara. "Ananipenda. Mungu ananipenda sana. Ananipenda. Ananifikiria asubuhi ya leo. Ananitendea mambo mema asubuhi ya leo. Ameniwekea mpango."

Sababu ya kuwa na uhakika kwamba nitafanikiwa ni kwa sababu ananipenda. Nikihitaji kitu, ataniambia. Nisipokipata, ataniambia tena. Nisipokipata kwa muda wa miezi mitatu, ataniambia kwa mara ya tisini na tatu. Kukiwa na uhitaji, anaweza kupaaza sauti. Ikihitajika, atatuma watu wanne karibu nami na kusema, *Keith… acha nikuchoree picha hapa...* Ninaamini atanifanyia hivyo. Sizungumzii juu ya kujaribu; ninazungumzia ikiwa ninaihitaji. Nikijikwaa kidole cha mguu wangu na kuanguka, ninaamini ataniinua. Nikichukua mkondo mbaya, atanishika na kusema, *Keith, si hivyo; njia ni hii.* Atanisaidia. Atanifundisha. Atanirekebisha. Ataniongoza. Atafanya hivyo kwa sababu ananipenda.

Ikiwa kweli unaamini hili, unawezaje kusema, "Sidhani ataniponya"? Hilo ni jambo lenye kupingana. "Loo, ananipenda, lakini sidhani kama atanisaidia kulipa gharama za nyumbani kwangu." Hilo haliwezi tendeka, sivyo? Ikiwa ananipenda, atanisaidia—na tayari amenisaidia.

Mungu anatupenda. Ninataka kukupa baadhi ya sababu kwa nini tunajua kwamba Mungu anatupenda—na hakuna umuhimu fulani kwa utaratibu huu.

**Sababu ya Kwanza: Tunajua Mungu anatupenda kwa sababu biblia inatuambia hivyo.**

Acha nitilie maanani katika jambo hili: Yesu ananipenda, *labda* ni kweli? Hapana! Najua *hili kwa hakika* . Kwa nini? Kwa sababu ya biblia—hatuzungumzii kitabu kingine— *Biblia* inaniambia hivyo.

Yeremia 31:3 inasema, “BWANA akawatokea kwa mbali: Nimekupenda kwa upendo wa milele. Na hivyo kwa upendo usioshindwa, nimekuvuta kwangu.” Unauliza, “Bwana, unatupenda?” Anasema, “Ndiyo, nimekupenda kwa upendo wa milele. Ndiyo sababu nimekuvuta kwa fadhili zenye upendo.”

Miaka kadhaa iliyopita, nilikuwa sakafuni nikiomba na kufikiria, na Bwana akasababisha niweze kukumbuka mambo mengine. Alinionyesha kile alichonifanyia. Unaelewa, katika Yohana 15:16, alisema, “Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi na kuwaweka ninyi ili mwende mkazae matunda na matunda yenu yadumu. Kwa hiyo, chochote mtakachomwomba Baba kwa jina langu, atawapa.” Alisema mambo haya ili furaha yetu iwe kamili (mstari wa 11). Akasema, “Nilikuchagua wewe.” Na kwa hivyo nilikuwa nikifikiria, " *Niliitikia wito wa kuenda kwenye madhabahu* ." Alisema, "Keith, nilifanya kazi kwa miaka mingi ili kukufikisha mahali ambapo unaweza kusikia na kujibu." Naam, alifanya hilo.

Nikasema, “Tulienda kwenye Kituo cha Mafunzo ya Biblia cha RHEMA,” na Bwana akasema, “Keith, nilikuwa nikifanya kazi juu yako kwa miaka mingi ili kufikisha imani yako mahali ambapo ungeweza kuamini kwamba ningeweza kukuhudumia.” Naye akaongeza neema, na kuongeza nguvu, na akatupa lishe, na kutubeba juu ya mabawa yake ya mfano.

Ni mara ngapi tumefikiri kwamba “tulikuwa tukitenda mema katika imani yetu,” na tulikuwa tukifanya vizuri tulivyojua, lakini kama tungeona yote kwa kina, tungeona kwamba alikuwa ametubeba? Akasema, “Ndiyo, nimekupenda wewe.”

Kuna mengi katika Injili ya Yohana kuhusu hili, na vilevile katika Yohana wa Kwanza. Yesu alizungumza katika Yohana 16:27, na tunajua alichosema ni sawa na kweli. Alisema, “Baba mwenyewe anawapenda ninyi, kwa sababu ninyi mmenipenda mimi na kusadiki kwamba nilitoka kwa Mungu.”

Katika Yohana 17, Yesu anaomba. Je, unaamini kuwa sala yake inajibiwa? Katika Yohana 17:23, Yesu alisema, “Mimi niko ndani yao na wewe ndani yangu ili wafanywe kikamilifu umoja. Ndipo ulimwengu utajua kwamba wewe ulinituma na kwamba umewapenda wao kama vile ulivyonipenda mimi.” Je, unaona hilo? Yesu alisema, “…ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe uliyenituma, na ulimwengu ujue ya kuwa umewapenda wao kama ulivyonipenda mimi. Je, unaamini kwamba Baba alimpenda—na anampenda—Yesu? Kwa kweli, si kila siku unasikia sauti ya Mungu kutoka mbinguni ikisema, “Huyu ni mwanangu mpendwa, ninayependezwa naye.” ( Mathayo 3:17 ) Lakini hapa anatuambia kwamba sasa, akiwa ndani yake, anatupenda sisi kama vile anavyompenda. Usijiwekee mzigo mkubwa wa kuelewa hili—liamini tu kwa imani.

Sema hili kwa sauti: **"Ananipenda kama vile anavyompenda Yesu."**

Anataka ulimwengu ujue hili. Anataka ulimwengu ujue kwamba anakupenda na ananipenda mimi kama vile anavyompenda Yesu.

1 Yohana 3:1 inasema, "Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu…" Sasa huo ni upendo. Mimi ni mwana wa Mungu. Wewe ni mwana wa Mungu. Mwanamume kwa mwanamke, sisi sote ni wana wa Mungu.

Alisema katika Ufunuo 3:9 , "Kwa sababu hiyo nitawatoa watu wa sinagogi la Shetani, (wanaosema kuwa ni Wayahudi, nao sio Wayahudi, bali waongo), nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako, na kutambua kwamba nimekupenda. Ndiyo, huenda tukachambuliwa sasa, na tunaweza kudhihakiwa, kuteswa, na kuitwa "wanyonge." Tunaweza kuitwa "dhaifu," na tunaweza kuitwa "wajinga," lakini kabla jambo hili halijaisha, adui zetu watawekwa chini ya miguu yetu, na atamfanya kila mtu aone kwamba anatupenda. Alituchagua sisi.

Hio itakuwa njia yetu ya kudai umaarufu. "Wewe ni nani?" Mimi ndiye anayempenda. Kuhusu watu waliokuwa maarufu na waliojiinua sana, wenye kiburi na wakaidi, walioasi na walionena matamko ya kukufuru kanisa lake, atawaleta na kuweka nyuso zao chini moja kwa moja kuelekea miguu yako na kusema, "Unaona sasa: ninawapenda." Kisha tutasema, "Ndio, ananipenda. Nilikuambia!"

Hatupaswi kujitetea au kujihesabia haki. Hatupaswi kuwashawishi watu wengine kwamba anatupenda. Yeye atalidhihirisha mwenyewe. Anafanya papa hapa na sasa kwa ulinzi wake, kwa upendo wake, na kwa baraka zake. Kadiri unavyotembea karibu na Mungu, ndivyo anavyoweza kudhihirisha upendo wake maishani mwako, hadi inakuwa dhahiri zaidi na zaidi kwa watu wanaokuona kuwa Mungu anakupenda. Anataka kuonyesha kwamba anawapenda, pia, kama watamruhusu. Anafurahia kutubariki. Tunajuaje kwamba Mungu anatupenda? Alituambia kuwa anatupenda.

**Sababu ya Pili: Upendo wa Mungu kwetu ni dhahiri tangu kuumbwa kwa ulimwengu.**

Alituumba kwa mfano na sura yake. Biblia inatuambia, "Tangu kuumbwa kwa ulimwengu, sifa za Mungu zisizoonekana—nguvu za milele za Mungu na asili yake ya kimungu—zimeonekana waziwazi, kwa sababu zinaeleweka kupitia vitu ambavyo Mungu ameumba." ( Warumi 1:20 ) Katika Mwanzo 1:31 , linasema, Mungu akaona kila kitu alichokifanya: kilikuwa chema sana. Na kwa kweli *ni* vyema mno!

Kuna baadhi ya wanasayansi walio kama vipofu na waliochanganyikiwa, watafiti, na wanafalsafa ambao wanajaribu kwa nguvu zao zote kuwasadikisha vijana wetu, watoto, na vijana wetu kwamba sisi si wa maana sana—kwamba Dunia si jambo kubwa kiasi hicho katika ulimwengu. Wanasema kwamba sisi wanadamu ni wanyama walio bora kwa sababu ya mageuzi, hatuko muhimu zaidi kuliko nyani, na kwamba dunia sio ya kipekee zaidi kuliko sayari nyingine yoyote. Kuna galaksi nyinginezo, na sisi sio muhimu sana.

Kila kitu kinalenga kutufanya tujisikie kuwa sisi si wa maana. Je, unadhani fikira hio ilitoka wapi? Ilitokana na shetani. Nakuhakikishia kwamba shetani anatuonea wivu. Alikuwa katika uwepo wa Mungu. Anajua jinsi ilivyo kuwa katika upendo huo na uwepo huo, lakini ameupoteza

kwa sababu ya kiburi chake na uasi—na hawezi kuurudisha. Sasa wewe na mimi tu ndio tamaa yake kuu. Tumekusudiwa kuwa katika upendo wake kwa umilele, na shetani hawezi kustahimili hilo.

Watu wanatucheka kuhusu hili, lakini wacha niwaambie, na ninasema bila kuomba msamaha—sisi *ni* hamu yake kuu. Sababu ya sayari hizo zote kuwepo ni ili dunia iweze kuwepo. Sababu ya dunia kuwa hapa ni ili tuwe hapa. Aliiumba kwa ajili yetu. Ndio maana kuna jua. Ndio maana kuna mwezi. Ndiyo maana kuna sayari nyingine. Nazo ziko kwa ajili yetu.

Wanasayansi watasema, "Majivuno gani haya. Ujinga ulioje." Hapana, *ni* wapumbavu. Sababu ya jua kuwaka asubuhi hii ni kwa ajili yako! Sababu ya ulimwengu kugeuka ni kwa ajili yako! Sababu ya kwamba bahari inakuja dhidi ya mchanga ni kwa ajili yako! Dunia jinsi ilivyo sasa si kama ilivyokuwa wakati ilipoumbwa hapo awali. Imezoroteka. Imeharibika sana. Lakini hata katika hali yake ya kuzoroteka, baadhi ya uzuri wake wa awali umebakia. Ikiwa utasikiliza kwa moyo wako na utaangalia, kila nyota inayometa inasema, *Ninakupenda.* Kila wimbi linasema, *nakupenda.* Kila ua, kila mti, kila kitu, kila kiumbe katika uumbaji unasema, *Nakupenda. Nilifanya haya yote kwa ajili yako. Nilikuumba na nilifanya hivi kwa sababu ninakupenda. Nakupenda.* Ndio maana upepo unavuma. Ndio maana naweza kuvuta pumzi nyingine. Sikiliza moyo wako. Unasema nini? Mungu anasema, *nakupenda.* Alituumba.

**Sababu ya Tatu: Tunajua kwamba Mungu anatupenda kwa sababu ya ukombozi.**

"Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." ( Yohana 3:16 )

Andiko la Waroma 5:8 linasema, "Mungu hutushangilia," au huonyesha, "pendo lake kwetu sisi, kwa kuwa, tulipokuwa tungali watenda-dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu."

Waefeso 2:4-5 inasema, "Hata hivyo, Mungu ni mwingi wa rehema. Alitupa uhai kupitia Kristo tulipokuwa wafu kwa sababu ya mambo mabaya tuliyofanya. Alifanya hivyo kwa sababu ya upendo mkubwa alionao kwetu."

Ufunuo 1:5 inasema, "Kristo… Yule anayetupenda na kutuweka huru na dhambi zetu kwa damu yake."

Biblia pia inasema, "Upendo hufunika wingi wa dhambi." ( 1 Petro 4:8 )

Kupitia dhambi, mwanadamu alikuwa amejiuza, amepoteza nafasi yake mbele za Mungu, amepoteza mamlaka yake, na kupoteza umiliki wake katika dunia. Lakini Mungu hangeruhusu hali ibaki hivyo kwa sababu alitupenda sana. Ilibidi atukomboe. Ilibidi aturekebishie mambo. Hakuweza kuvumilia. Hangeweza kuvumilia kuona kwamba tulitengwa naye, tukadunishwa, tukawa bila lolote, na kushushwa chini. Ilimbidi ayafanye mambo jinsi alivyokusudia. Yaani, tuwe katika uongozi wake, familia yake yote, tukitawala na kuongoza. Kwa hiyo alikuwa na mpango, na alidumu na mpango huu wa upendo kwa karne nyingi, ingawa ulionekana kuwa haungetimia, na Shetani alikuwa akipigana nao. Alikuwa na manabii waliotoa utabiri, na aliwapa

malaika wake kazi. Alihakikisha kwamba mpango wake ulitukia wakati uliopaswa, na kwamba kila kitu kilijipanga kuhakikisha utimizo wa mpango wake.

Katika utimilifu wa wakati, Yesu alizaliwa kutoka kwa mwanamke, na Mungu alionyesha ukamilifu katika ulimwengu wa kimwili. Kuzaliwa kwake kulisema kwa ulimwengu, "Nakupenda." Kila ujumbe wake ulikuwa katika upendo na wema. Wakati huo, watu walikuwa wamezoea tu kusikia Sheria. Wakati fulani walisikia tu tafsiri ya kisheria ya hukumu ya Mungu. Ilizungumzwa zaidi kuliko kitu kingine chochote. Lakini hapa, asili ya kweli na kamili ya Mungu inafunuliwa wakati mtu anakamatwa katika tendo la uzinzi: "Yeyote ambaye hakutenda dhambi na arushe jiwe la kwanza." ( Yohana 8:7 ) Wote wakaondoka. Yesu akamtazama yule mwanamke na kumwuliza, "Hakuna mtu aliyekuhukumu?" Alisema, "Hapana." Akasema, "Wala mimi sitakuhukumu, nenda zako na usifanye dhambi tena." Halleluyah. Yesu hakuja ulimwenguni ili kuuhukumu ulimwengu, bali ili sisi tupate kuokolewa. Ukombozi ulioje! Alitununua tena kwa kitu cha thamani sana alichokuwa nacho. Hatukukombolewa kwa fedha na dhahabu. Tulikombolewa kwa damu ya thamani ya Mwana-Kondoo ambayo ina uzima wa Mungu ndani yake. Uhai wenyewe wa Mungu ulimwagwa kwa ajili yetu.

Kwa upande mwingine, shetani huja na kujaribu kutuambia kwamba sisi si wa maana. Lazima uwe mpumbavu sana kuamini uwongo huo, sivyo? Ikiwa hatufai, kwa nini Mungu atoe thamana kubwa kwa ajili yetu? Hatuzungumzii kuhusu dola milioni, au dola bilioni, au dola trilioni. Dhahabu yote duniani haiwezi kununua nafsi moja tu. Hakukuwa na kitu chochote katika ulimwengu ambacho kingeweza kununua nafsi isipokuwa damu ya thamani ya Mwana-Kondoo. Naye akalipa. Aliimwaga na akalipa thamana hio. Kwa nini? Anakupenda. Anataka uwe wake na alikuwa tayari kulipa chochote ili akurudishe. Je, ulisoma hilo? Alikuwa tayari kulipa *chochote* .

Unajua thamani ya kiasi kilicholipwa? Yesu ni mwenye nguvu kuliko mtu yeyote utakayewahi kuona na kusikia, lakini katika bustani, alikuwa akitokwa na jasho la damu. Alisema, “Ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke. ( Mathayo 26:39 ) Lakini hakukuwa na kitu kingine chochote ambacho kingeweza kutununua. Hakuna chochote kingine kingetukomboa. Kwa hiyo Baba akasema, *Nawataka. Lazima wawe wangu. Nina hamu kubwa ya kuwafanya wangu. Fanikisha mapenzi yangu.*

Yesu alijua, *itatugharimu kila kitu* , lakini Baba alisema, *Fanikisha hili.*

Yesu alijua ni bei kubwa sana, lakini Baba yake alisema, *Lipa fidia hii, kwa sababu ninataka kuwakomboa* .

Sema hivi kwa sauti: **“Ananipenda. Ananipenda."**

Je, alilipa fidia kubwa kwa ajili yetu? Warumi 8:31-32 inasema, “Basi tuseme nini juu ya mambo haya? Ikiwa Mungu yuko upande wetu, ni nani atakayekuwa dhidi yetu? Hakumhurumia mwana wake mwenyewe bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote. Je, hatatupa sisi vitu vyote pamoja Naye?”

Rafiki, kama Mungu angewahi kukuzuilia chochote, ingekuwa ni mwanawe. Kama Mungu angelisema, *Hapana, siwezi kumtoa mwanangu kama dhabihu. Sitawapa hio fidia,* ingekuwa ni

Mwanawe—Mwanawe wa pekee. Mstari wa 32 unasema, “Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?" Ikiwa alikupa Yesu, atakupa nyumba. Ikiwa alikupa Yesu, atakupa gari. Ikiwa alikupa Yesu, atauponya mwili wako. Alipotupa Yesu, alitupa mambo haya yote, pamoja naye. Ndiyo maana alisema, “Vitu vyote ni vyako.”

Je, unaweza kuona jinsi shetani amelipumbaza na kulidanganya Kanisa? Baadhi ya watu husema, “Sitaki kumsumbua Bwana kwa sababu ya hilo… sijui kama ni mapenzi ya Bwana…” Hawana tu sehemu ndogo ya fikira jinsi yeye anatupenda. Tayari ametuonyesha jinsi anavyotupenda: Alitupa Yesu. Ndivyo ilivyo. Ikiwa atatupa sisi Yesu, “… atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?” Haleluya! Alitupa kila kitu!

Nimeguswa na yale yaliyotukia katika Yohana 20:17, wakati Yesu alipofufuliwa mara ya kwanza kutoka kwa wafu, na wanawake walikuwa pale na wakamwona. Wakaanguka miguuni pake ili kumwabudu, naye akasema, “Usinishike, kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba…” Akawaambia “Nendeni kwa ndugu zangu na dada zangu mkawaambie. , ‘Ninapanda kwenda kwa Baba yangu na Baba yenu, kwa Mungu wangu na Mungu wenu.’”

Fidia imelipwa, na amepaa juu, kuwa mpatanishi wetu. Alitoa damu yake mwenyewe katika Patakatifu pa Watakatifu na kupata ukombozi wa milele. Anawaambia, “Nendeni mkawaambie ninaenda kwa Baba Yangu na Baba yenu, Mungu Wangu na Mungu wenu. Kwa sababu ya kile alichokifanya, ninaweza kusema kwamba yeye ni Baba yangu vile tu yeye alivyo Baba ya Bwana Yesu, na yeye ni Mungu wangu, kama vile yeye ni Mungu wa Yesu—na ananipenda kama vile anavyompenda Yesu.

Wengine husema, “Sijui kama ninaweza kuamini hilo. Sioni jinsi hilo linaweza kuwa halisi." Kuna mambo mengi ambayo huwezi kuona, lakini unaweza kuamini. Ni bora kuacha kusababu na kuelewa kindani, bali uamini tu.

Unaweza kuuliza, “Ninawezaje kujua nimeamini kikweli?” Moyo wako utaathirika. Imani yako itaanza kujitokeza, na mambo ambayo yalionekana kuwa makubwa hayataonekana kuwa makubwa sana. Mambo ambayo uliwahi kutoamini, hutasaili tena kuyahusu. Kwa nini? Kwa sababu ikiwa alikupa Yesu, atakupa kitu chochote kizuri.

**Sababu ya Nne: Tunajua kwamba Yesu anatupenda kwa sababu bado anatoa.**

Ingawa alijitoa mwenyewe na tone lake la mwisho la damu, na alilipa gharama kamili alipofufuliwa kutoka kwa wafu, huo sio mwisho. Bado anatoa.

Waebrania 7:25 inasema, “Ndiyo maana anaweza kuwaokoa kabisa wale wanaomkaribia Mungu kupitia yeye, kwa maana yu hai sikuzote ili kusema na Mungu kwa ajili yao.”

Yesu alikuwa kwenye mlo wa mwisho wa Pasaka pamoja na wanafunzi wake kabla tu ya saa zake za mwisho duniani. Wakati fulani katika chakula cha jioni, alisimama, akavua vazi lake, na kujifunga taulo kama mtumwa. Alichukua beseni la maji, na akaenda kwa wanafunzi wake.

Sasa usisikie tu haya kidesturi. Yesu aliye Bwana, Mwana wa Mungu, Kichwa cha Kanisa, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana—alivaa taulo, akapiga magoti mbele ya wanafunzi wake, akachukua maji, na kuanza kuwaosha miguu. Alienda kutoka mmoja hadi mwingine, kisha aliyefuata. Alimfikia Petro, na Petro akasema, "Hapana! Hutaiosha miguu yangu." Unaweza kuelewa kwa nini Petro angehisi hivyo. Tunamzungumzia Yesu, akiwa amepiga magoti mbele yako na kuosha miguu yako. Yesu alisema, "Ninyi hamjui ninachofanya sasa, lakini mtajua baadaye." Petro akasema, "Hapana. Hunioshi miguu." Yesu alisema, "Kama sifanyi hivyo, basi huna sehemu yoyote na mimi." Hii ni sababu moja ya Bwana kumpenda Petro—kwa sababu alisema, "Sawa, nioshe. Osha miguu yangu. Nioshe." Petro alikuwa mwepesi wa kutubu.

Yesu alisema, "Sikuja ili wengine wanitumikie. Nimekuja kutumikia." ( Yohana 10:45 ) Ikiwa huo si upendo, rafiki yangu, ni nini? Mfalme wa wafalme yu hai siku zote ili atoe dua kwa ajili yako na mimi. Kila mchana na usiku, yuko kwenye mkono wa kuume wa Baba. Yeye ndiye mtetezi wetu, wakili wetu na mwakilishi wetu. Anatuona kuwa wake. Anasimama kwa ajili yetu. Anazungumza kwa niaba yetu. Yeye ndiye mtume na kuhani mkuu wa maungamo yetu. Tunakiri jambo fulani kwa imani, naye anatuunga mkono na kusema, "Ndiyo." Yeye ndiye mpatanishi kuhusu imani yetu na maungamo yetu. Hii ni kila siku. Anatupenda, na anatujali.

**Sababu ya Tano: Tunajua Mungu anatupenda kwa sababu ya zawadi kuu alizotupa.**

Mungu ni mpaji-zawadi, mpaji mkuu. Zawadi kubwa zaidi ambayo nimezungumza ni Yesu. Alitupa Yesu, lakini huo haukuwa mwisho. Pia alitupa roho mtakatifu. Hatuzungumzii gari jipya au nyumba. Alitupa roho mtakatifu. Kila wakati unaposema katika ndimi, Mungu anasema, *Nakupenda. Ndiyo maana nilikupa roho mtakatifu.* Kila wakati unapohisi utiwa mafuta juu yako, anasema, *Ninakupenda.*

Yesu aliwatazama wanafunzi wake kabla hajaondoka na kusema, *Wanaume, ninyi nyote mnahitaji msaada. Lakini sitawaacha kama mayatima. Sitawaacha hoi. Nitaomba kwa Baba, kwa maana ninawapenda, naye atawapa msaidizi mwingine. Atakaa nanyi milele. Atakuwa ndani yenyu na juu yenyu. Yeye atawafundisha, atawaongoza, na kuwaonyesha mambo yajayo. Atakusaidia kuhubiri, kuomba, kutabiri, na kurembesha nywele zako asubuhi. Atakusaidia kuendesha gari hadi kazini. Kwa sababu anakupenda, atakusaidia, kwa muda wote utakaokuwa hai. Atakuwa ndani yako. Utakuwa na msaada wa mara kwa mara.* Ndio, anatupenda. Alitupa roho mtakatifu, lakini si hilo tu. Ukiwa na roho mtakatifu, unahitaji kujumuisha zawadi zote na maonyesho ya roho. ( 1 Wakorintho 12 ) Kwa nini alitupa maneno ya ujuzi? Anatupenda. Kwa nini alitupa maneno ya hekima na utambuzi wa roho? Kwa sababu anatupenda. Kwa nini alitupa kipawa cha uponyaji? Anatupenda. Na kuna zaidi.

Kristo alipopaa mbinguni, alitoa zawadi kwa wanadamu. Waefeso 4:11-12 inasema, "Naye alitoa wengine kuwa mitume, wengine manabii, wengine wainjilisti, na wengine wachungaji na waalimu. Kusudi lake lilikuwa kuandaa watu wa Mungu kwa ajili ya kazi ya kutumikia na kujenga mwili wa Kristo." Kwa nini?  Kwa sababu anatupenda. Alitupa zawadi hizi, na kila wakati zinatumiwa, unapaswa kuzifikiria kama zawadi iliyofunikwa vizuri. Hatuzungumzii juu ya kisanduku kidogo chini ya mti wa Krismasi; tunazungumza juu ya wanadamu, karama za kiroho, karama za huduma.

Sulemani alipoanza kutawala katika ufalme wa Daudi baba yake, alimwambia Hiramu—ambaye alimpenda Daudi sikuzote—kwamba alitaka mierezi na vitu vingine vya kujenga nyumba ya Mungu. Hiramu akatuma mjumbe na kusema, "Solomoni, unajua ni kwa nini Mungu amekufanya mfalme? Ni kwa sababu anawapenda watu hao." ( 2 Mambo ya Nyakati 2:11 ) Mungu aliwapa mfalme mwenye hekima.

Alitupatia mitume na manabii. Wao ni zawadi kwa mwili wa Kristo, na Mungu anafichua, anafunua, na kujidhihirisha mwenyewe kupitia karama hizi. Hizi ni zawadi kwako.

Watu kama Ndugu Kenneth Hagin walitumwa kwa sababu Mungu anatupenda. Alisema, *ninawapenda sana, nitawapa zawadi kubwa. Ninaweza kuwapa nini? Nitawapa baadhi ya mitume—hiyo ni karama kubwa—na manabii, wainjilisti, wachungaji na walimu. Nitawapa zawadi za kikweli.* Mungu anajua jinsi ya kutoa zawadi.

Anatupa karama za kutusaidia, kutufundisha, kutupa njia, kutuongoza katika maombi, kututabiria, kutujenga, kutufunza, kuturekebisha, na kutupa maagizo. Kwa nini? Anatupenda. Kila wakati tunapomwona mtu akiwa kwenye jukwaa, tunapaswa kuwa tunamsikia Mungu akisema, *Ninakupenda. Ndio maana nimewatuma hapa. Ndiyo maana nilikupa wewe, kwa sababu ninakupenda.*

Sema hivi kwa sauti: **"Ananipenda. Ananipenda."**

**Sababu ya Sita: Tunajua anatupenda kwa sababu ya ulinzi na utoaji wake unaoendelea.**

Bila ulinzi wake, unajua ni mara ngapi ungekuwa umeuawa kufikia sasa? Kuanza, fikiria ulipokuwa na umri wa miaka miwili. Ni mara ngapi malaika mlinzi alikuelekeza katika njia hii badala ya ile? Ulikaribia kuondoka ukingoni, na yeye akakuvuta nyuma. Mambo mengi hutokea ukiwa mdogo, mambo ambayo hata huyakumbuki. Ni mara ngapi amekulinda na kukuepusha na hatari? Kuna mambo mengi hata huyajui kwa sababu hayakutokea. Hukujua kutoka kwa kile ulichoepushwa kila siku. Ibilisi yuko nje akijaribu kutuua, lakini ikiwa tutatembea na Mungu, hawezi kutugusa. Bwana hutusaidia kushinda kila mpango na kila kitu shetani anajaribu kufanya. Anatulinda, hutuinua juu, hutulinda, na hutuongoza.

Kuhusu riziki, je, amekidhi mahitaji yzko? Kupitia kila mlo unaokula, anasema, *Nakupenda.* Kupitia kila kila vazi ulilo nalo, Mungu anasema, *nakupenda.* Je, una mahali pa kupumzika na kulala? Mungu anasema, *nakupenda. Ninakutunza. Nitaendelea kukutunza.* Mungu anatupenda.

**Sababu ya Saba: Tunajua Mungu anatupenda kwa sababu ya mashirika yetu—familia yetu na marafiki zetu.**

Katika kitabu cha Matendo, kinarejelea "mashirika yako mwenyewe." (4:23) Hii ni miunganisho ya kimungu. Unaweza kufikiria kuwa watu wanakupenda na kujihusisha na wewe kwa sababu ya haiba yako, au kwa sababu wewe ni mzuri sana, lakini nitalazimika kutuliza kiburi chako. Waisraeli waliambiwa wakati mmoja, katika Kumbukumbu la Torati, "Usifikiri kwamba Mungu alikuchagua kwa sababu *yako* . Haikuwa kwa sababu ulikuwa hodari zaidi; mlikuwa wachache

zaidi. Haikuwa kwa sababu ulikuwa mkubwa sana; ulikuwa muasi. Ni kwa sababu aliwaahidi baba zenu.” ( 7:7-8 ) Anakupenda na kukuchagua wewe. Alituchagua sisi.

Je! una marafiki wazuri na familia nzuri? Unaweza kujisikia kama una aina nyingine, pia, lakini wanaweza kubadilika. Je, una baadhi ya watu ambao wanakupenda na kujali kama utakuwa hai au utakufa? Hiyo ni zawadi kutoka kwa Mungu.

Je, una marafiki wowote ambao wapo kwa ajili yako kila wakati? Wale ambao ukiwapigia simu alfajiri, na watakuja kukuchukua. Ni marafiki ambao watakusaidia kila wakati. Hiyo ni zawadi. Sio kwa sababu wewe ni bora na wakuvutia zaidi. Ni kwa sababu Mungu anakupenda na anataka uwe na rafiki—mtu ambaye atakuwa pamoja nawe ili usiwe peke yako. Kuna baadhi ya watu ilibidi Mungu awalete kwenu kwa njia isiyo ya kawaida. Hawangekuangalia wewe, na wakafikiri, *siwajali sana,* lakini basi yeye aliwaleta kwako, na mara moja, kwa sababu fulani wanakupenda. Hawajui kwa nini wanakupenda, lakini wanakupenda kikweli. Ni kwa sababu Mungu anakupenda ndio maana alikupa marafiki.

Alikupa watu ambao wangekutolea sala. Kuna watu wengi sana duniani wanaohitaji maombi, hivyo mtu anapokuombea badala ya yeye au mtu mwingine, hicho ni kibali; hiyo ni zawadi. Anakupa marafiki ambao watatumia wakati wao na wewe, watakutumia pesa, kukununulia chakula, au kukununulia nguo. Huyo ndiye Mungu. Asili ya mwanadamu ni ya ubinafsi, na hata wakristo wengi ni wa kimwili sana. Lakini Mungu anapowavuta watu kwako nao wanakusanyika kwako, wanakukumbatia, na kusema, “Lo, tunakupenda. Sisi ni marafiki zako,” Mungu anakupenda. Anakutegemeza, anakusaidia, na kukutia moyo kuwapitia.

Umewahi kuwa na wakati ambapo hukuwa na uzoefu bora zaidi ulimwenguni, na mtu akajitokeza na kusema jambo sahihi tu, kwa wakati unaofaa?

Wahubiri huwa hawapati barua nzuri. Wakati mwingine kuna barua mbaya. Nimepokea barua kutoka kwa watu wakiniambia kwamba napaswa kuufanyia ulimwengu jambo jema kwa kuacha huduma, kwa kuwa ninaumiza watu. Wamesema kwamba ninawadhuru watu, na ikiwa ninawapenda, niache kuhubiri.

Wakati fulani shetani huwachochea watu ili wajue la kusema. Mara nyingi ni jambo lisilo sahihi kwa wakati usiofaa. Ukiwasikiliza, utaanza kuvunjika moyo.

Lakini Mungu anakupenda sana hivi kwamba atawafanya marafiki zako wanne wajitokeze kwenye mlango wako na kusema, “Wewe ndiye bora zaidi. Pongezi kwako! Na tunakupenda. Umetiwa mafuta. Wewe ni mtu wa Mungu. Una neno kwa sasa." Atakutegemeza, atakusukuma, atakujenga na kukusaidia. Kwa nini atafanya haya yote? Kwa sababu anakupenda.

**Sababu ya Nane: Tunajua Mungu anatupenda kwa sababu ya sala zetu zote ambazo amejibu, na nyakati zote ambazo ametuandalia yote tunayohitaji.**

Unawezaje kutilia shaka upendo wake kutuelekea? Unachotakiwa kufanya ni kufikiria kidogo tu. Ni mara ngapi umeomba, wakati mwingine ukiwa na imani ndogo, lakini ilikuwa bora zaidi uliyojua wakati huo? Ulizunguka huku na huku, hukuweza kuweka andiko moja pamoja na

lingine, na ukawa utendaji wa kusikitikiwa. Lakini ulikuwa ukifanya kilicho lingana na uwezo wako wakati huo, na kwa hiyo Mungu akasema, *Hilo ni jaribio zuri. Haya, twendelee.* Watu wanazingatia uhalali kwa kiasi kikubwa. Wanaogopa kwamba ikiwa hawataungama mara arobaini na tatu kabla ya chakula cha mchana, na ikiwa hawatasema sawasawa na Biblia ya King James Version, kutakuwa na mwanya fulani wa kisheria, na watakuwa wamepotoka. Hapana! Mungu anaona moyo wako. Imani ni ya moyo. Hiyo ina maana unaweza kuomba isivyo kawaida, ukose kujieleza vema, na kuyasema kwa maneno yasiyo fasaha, lakini Mungu anasema, "Ninajua unachomaanisha."

Kumekuwa na nyakati ambapo nilikuwa nikiamini kwa ajili ya jambo fulani, na nilisema jambo lisilofaa na nilikuwa namna fulani ya kudai jambo lisilofaa. Lakini basi jambo lililo sawa likatukia, na nikagundua, *Naam, ni hivyo nilimaanisha. Ulijua nilichomaanisha. Ulijua nilisema isivyofaa. Samahani.* Naye akasema, *Ndio, nilijua ulichomaanisha.* Utukufu ni wake! Ni kwa sababu ananipenda.

Msifu Mungu na kumshukuru kwa sababu anakupenda. Hatuzungumzii mtu mwingine: ni wewe — Anakupenda .

Alisema, "Ndiyo, nimekupenda kwa upendo wa milele. Ndiyo sababu nimekuvuta kwa fadhili zenye upendo." ( Yeremia 31:3 ) Ni wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu. ( Warumi 2:4 ) Ni fadhili za Mungu.

Ibilisi anajaribu kufanya yote awezayo ili kutufanya tukubali ubinafsi, kuchanganyikiwa hadi tusifikirie kuwa hatuna kitu cha kushukuru. Watu wanaweza kufikia mahali wanapofikiri, *Mungu hanijali kabisa.* Huu ni uwongo mkubwa sana unaoweza kusikia au kuamini. Siamini. Ninakataa kukubaliana nalo hata kwa muda mchache. Mungu amethibitisha upendo wake kwangu. Kamwe nisikosoe wala nisitilie shaka kwa dakika moja. Kuuliza nia yake ya kutupenda ni kumtilia shaka.

Upendo wake unapozidi kuwa na nguvu ndani yako, unauondoa woga, na unatambua utafaulu.

Sema hivi kwa sauti:

**Sitakufa; mimi naenda kuishi.**
**Sitakumbana na hali ngumu za kifedha; nitafaulu.**
**Familia yangu haitapitia magumu; tutafanikiwa.**
**Watoto wangu watafanikiwa. Ndoa yangu inaenda kufanikiwa.**
**Huduma yangu itafanikiwa. Kanisa langu litafanikiwa.**
**Nitafanikiwa kwa sababu Mungu ananipenda.**
**Ananipenda, na ninaweza kumtegemea. Haleluya!**

Iseme sala hii:

> **Baba, nakushukuru kwa wema wako. Asante kwa upendo wako. Ninaomba uendelee kufunua mambo haya moyoni mwangu, unifanye niyakumbuke, na unisaidie kuona kwa uwazi, nifanye nione jinsi unavyonijali kweli. Nisaidie kuona ni kiasi gani umenifanyia na unanifanyia, na yote unayopanga kunifanyia. Nisaidie**

**kukiweka kipaumbele changu milele na kuishi katika utakatifu. Bwana, nakushukuru kwa kunipenda. Nakupenda. Asante kwa yote ambayo umenifanyia. Asante kwa kunipenda hivyo. Nakupenda.**

# Mungu **Ananipenda**

Mungu anakupenda. Anakupenda kweli kweli - kama vile anavyompenda Yesu  Na unapojua anakupenda, inakuondolea maswali mengi, kufadhaika, na kuyumba-yumba.

Imani yako inainuka, na unajua utafanikiwa - si kwa sababu wewe ni wa ajabu, lakini kwa sababu anakupenda!



Keith Moore ndiye mwanzilishi na rais wa Kanisa la Moore Life Ministries na Faith Life la Branson, Missouri na Sarasota, Flordia.

Kitabu hiki kimeletwa kwako bila malipo na washirika wa Kanisa la Moore Life Ministries/Faith Life.

*Moore Life Ministries*
6009 Business Blvd.
Sarasota, FL 34240
(941) 702-7390 | www.flintl.org

NO CHARGE - SEED
BK25
ISBN: 978-1-940403-01-4